

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 8 Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Kikao chetu leo cha Arobaini na Saba. Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 396

**Ukarabati wa Barbara Zilizoharibiwa na
Mvua katika Wilaya ya Hanang**

MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y. MHE. DKT. MARY M. NAGU) aliuliza:-

Katika msimu wa mwaka 2015/2016, Wilaya ya Hanang ilikumbwa na mvua kubwa sana iliyosababisha kuharibika kwa miundombinu ikiwemo ya barabara.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(b) Je, ni lini Serikali itajenga na kukamilisha barabara iliyofunguliwa na Wachina inayopita katika Vijiji vya Mig'enyi, Milongoli, Gawidu hadi Ngamu na barabara inayounganisha Sechet, Wilaya ya Babati Vijijini kuititia Vijiji vya Basodesh, Basotu mpaka Mulbadaw?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizoharibika ziliandaliwa maombi ya fedha za dharura ambapo barabara ya Getasam – Mto Bubu ilikarabatiwa kwa shillingi milioni 438.259 katika mwaka wa fedha 2015/2016. Barabara ya Basotu – Basodesh katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilitengewa shillingi milioni 455 zilizotumika kujenga daraja moja lenye urefu wa mita 20 na kukarabati barabara hiyo urefu wa kilometra sita kwa kiwango cha changarawe.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari, 2018 Mfuko wa Barabara ulitoa fedha za dharura shillingi milioni 500 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Ming'enyi – Milongori. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019, barabara za Endasak – Gitting – Dawar – Gawal – Gawidu zimeombewa shillingi milioni 209 za kuzifanya matengenezo. Aidha, barabara ya Basotu – Basodesh imeombewa shillingi milioni 90 za kuwezesha ujenzi wa daraja linalounganisha Wilaya ya Hanang na Babati Vijijini.

MWENYEKITI: Ahsante. Hayo majina magumu eeh? Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Babati - Basodesh kuna korongo kubwa sana ambalo linawazuia watoto kwenda shule na kutokana na mvua hizi, ndiyo kabisa hali imekuwa mbaya. Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia watu hawa wa Hanang ili daraja au korongo hili likaweza kujengwa kwa sababu bajeti ya Halmashauri ya Hanang ni ndogo haiwezi kujenga barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Hanang na Jimbo la Mbulu Vijiji lilikuwa pacha. Kuna barabara nyingine inayotoka Dongobesh kupitia Maretadu kwenda Haydom hapitiki kabisa kwa sababu ya mvua hizi ambazo zimekuwa nyingi maeneo ya kule Mbulu. Je, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ina mpango gani wa kusaidia kukarabati barabara hizi ambazo mvua nyingi zimeharibu kabisa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba mvua zilizonyesha ni nyingi, mvua ni neema lakini wakati mwingine zikizidi pia zinaleta uharibifu mkubwa sana wa miundombinu. Kwa hiyo, kwa ujumla wake, naomba niwaagize Mameneja wa TARURA wa Wilaya zote mbili wakatazame uharibifu ulivyo, halafu waweze kushauri Serikali nini tuweze kufanya katika kusaidia ili wananchi waendelee kupata huduma.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sannda, atafuata Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi mvua za mwaka 2017 mwishoni na mwaka huu 2018 zimevuruga sana miundombinu katika Jimbo la Kondoa Mjini. Moja ya barabara iliyoharibika sana ni barabara ya Kingale ambapo

mpaka daraja lenye mawasiliano makubwa sana kati ya Kingale na maeneo ya jirani livilunjika. Daraja hilo limekuja kuangaliwa na watu wa *TARURA* Mkoa na watu wote wamelichunguza, mpaka sasa hivi bado halijafanyiwa kazi.

Je, ni lini sasa Serikali italeta mpango wa dharura wa kurudisha mawasiliano pale Kingale?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba tumekuwa na mvua nydingi ambazo zimesababisha uharibifu mkubwa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema katika swali lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pesa ya dharura ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya matengenezo ya dharura, theluthi mbili ya pesa hiyo imetumika katika kurudishia miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwa sababu uharibifu uliotokea kwa Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa mkubwa sana. Hata hivi leo hii navyoongea *almost* pesa yote iliyokuwa imetengwa ya dharura imeisha kwa sababu mvua zimenesha, miundombinu minge ikawa imeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Sannda na sababu sasa hivi na mvua nazo hata huko Kondoa hazinyeshi, kabla hatujaanza utekelezaji wa hiyo bajeti ambayo tulipitishiwa na Waheshimiwa na Wabunge, kama Serikali tutaona kuna haja ya kuchukua hatua zozote endapo maeneo hayo hayapitiki, tutafanya hivyo ili wananchi waendelee kupata huduma.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa niulize swali dogo la nyongeza.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kama alivyosema Naibu Waziri kwamba mvua za mwaka huu na miaka mingine zimekuwa zikileta adha kubwa sana kwa Jiji la Dar es Salaam.

Nataka Serikali ituambie, wana utaratibu gani sasa kuhakikisha kwamba miundombinu hasa ile ya mwendokasi pale walipoweka Makao Makuu pale Jangwani, inahamishwa ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Dar es Salaam wanapata usafiri bora, hasa ikizingatiwa kwamba Serikali iliwaondoa watu Jangwani lakini imejenga kituo kikubwa cha mwendokasi; ni lini mtakiondoa kituo kile?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimetangulia kutoa majibu yangu, mvua za safari hii zimekuwa nyingi ukilinganisha na miaka ya nyuma. Katika swalii lake anaongelea juu ya suala zima la kuondoa ile *stand au tuite garage* ya mabasi yaendayo kasi kwa maana ya pale Jangwani, lakini *issuesiyo* kuiondoa bali kuhakikisha kwamba miundombinu ipi inakuwepo ili hata kama mvua zikinyesha pale pasiweze kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mpango mahsus kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam wa kuhakikisha kwamba Bonde la Msimbazi linakuwa na miundombinu ambapo maji ambayo yatakuwa yanatoka kule juu yanaenda baharini kama ambavyo mkondo unaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa avute subira tarehe 20 Julai, kandarasi inafunguliwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miundombinu ile inakuwa na ukarabati ambao utakuwa ya uhakika kabisa. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mpakate.

Na. 397

Ahadi ya Kuanzisha Mkoa Mpya wa Selous

MHE. DAIMU I. MPAKATE (K.n.y. MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI) aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kuanzisha Mkoa mpya wa Selous.

(a) Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa mpaka wa Kusini wenye urefu wa zaidi ya kilometra 600 na wenye mikoa miwili tu sio salama kiulinzi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 15 Julai, 2013 Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ziarani Wilayani Tunduru alikutana na wazee wa Tunduru walioombwa mkoa mpya wa Selous. Katika majibu yake alielekeza taratibu zifuatwe kisheria, kwa maana hiyo, hakuahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo hayo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma imeratibu vikao kadhaa vyta kisheria kikiwemo Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa

wa Ruvuma cha tarehe 28 Novemba, 2017 kilichosositiza ombi la kuundwa kwa mkoa mpya wa Selous wenye Wilaya nne za Tunduru, Tunduru Kusini, Namtumbo na Sasawala, Tarafa 10, Kata 53 na Vijiji 212 kwenye eneo lenye kilometa za mraba 38,988 na idadi ya watu 499,913 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetafakari kwa kina maombi hayo na kuyaona kuwa ni ya msingi. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya kuimarishe kwanza miundombinu kama majengo ya Ofisi na nyumba za Watumishi na mahitaji mengine kama vifaa ya Ofisi, Watumishi wa kutosha na vyombo vya usafiri kwenye maeneo mapya ya utawala yaliyoanzishwa tangu mwaka 2010 na 2012, Serikali imesitisha uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala hadi maeneo mapya yaliyopo yalmarishwe kikamillifu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulinzi na usalama katika mpaka wa Kusini, ipo mikakati ya pamoja baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Msumbiji kuhakikisha kuwa mpaka huo upo salama. Nawaomba wananchi waendelee na shughuli zao bila wasiwasi wowote.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa eneo la Sasawala ndiyo eneo ambalo linategemewa kuanzisha Wilaya Mpya na Makao Makuu yake kuwa Lusewa; je, ni kwa nini Serikali isianzishe Jimbo jipya la Uchaguzi katika eneo hilo la Sasawala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilifuata utaratibu wote wa kuanzisha Wilaya mbili, kwa maana Wilaya ya Tunduru Kusini na Tunduru iliyopo sasa na kwa kuwa Halmashauri hiyo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

iliendesha vikao vya kuanzisha miji midogo miwili, katika Vijiji vya Nalasi na Mchoteka; je, Serikali haioni haja kwa sasa kuanzisha miji midogo katika eneo la Nalasi na Mchoteka? Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyeekiti, majibu yangu katika maswali yake mawili ya nyongeza, hayawezi kutofautiana sana na jibu langu la swalii msingi. Kuhusu kuanzisha Jimbo jipya, utaratibu wake uko tofauti kidogo na utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, suala la kuanzisha Jimbo jipya linahusisha sana Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi kabla ya michakato yoyote ya mikutano hajiaanza, inatakiwa itangaze nia ya kuanzisha Jimbo jipya katika eneo fulani, baada ya hapo ndiyo vikao viridhie na baadae Mheshimiwa Rais aridhie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, katika swalii lake la pili kwamba michakato ya kuanzisha Wilaya mbili kutoka katika Wilaya moja ya Tunduru, kwa maana Tunduru na Tunduru Kusini na miji aliyoitaja kwamba iwe miji midogo, utaratibu wake ni sawasawa na jibu langu kwenye swalii msingi kwamba hii miji midogo ni maeneo mapya ya utawala, kwa maana kwamba ukishakuwa na mji mdogo utakuwa na Halmashauri ya Mji, Mkurugenzi na utakuwa na vikao vinavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa hiyo, maeneo hayo yote ya utawala yamesitishiwa kuanzishwa hadi hapo tutakapoimarisha zaidi maeneo tuliyonayo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Jimbo la Mpanda Vijiji ni kubwa lenye kilometra za mraba 16,900. Jimbo hili limekuwa vigumu sana kurahisisha shughuli za kiutendaji kwa sababu ya ukubwa.

Je, ni lini Serikali itafikiria kuligawa Jimbo hili ili kupeleka huduma kwa wananchi kuwa karibu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hapa nchini yako maeneo ambako Majimbo yake ni makubwa sana pamoja na hili Jimbo ambalo Mheshimiwa Kakoso amelitaja.

Sasa utaratibu wake hautofautiani sana na maeleo ambayo nimeyatua hapo awali kwamba namuomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane, lakini hasa yeye kuwasiliana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili waingize kwenye orodha ya maeneo ambayo watayataja kwamba yanahitajika kugawanywa kuwa Majimbo mawili. Kwa hiyo, naomba sana tushirikiane baada ya hapa pengine tuonane ili tupeane maeleo zaidi.

MWENYEKITI: Haya tuone Selous, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini unaozungumzwa ilikuwa uchangiwe pamoja na Wilaya ya Liwale, Nachingwea na Masasi kutokana na mikoa hii kuwa mbali na Makao Makuu ya Mikoa. Serikali kusitisha uanzishwaji wa Mkoa huu wa Selous, huoni kwamba ni kuwanyima haki ya kimsingi wananchi wanaokaa maeneo haya ambao wako mbali sana na Makao Makuu ya Mkoa? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa MwenyeKITI, kwanza katika swali lake ameongeza maeneo ambayo hayajawahi kujadiliwa; yapo maeneo aliyoYaongeza hapa kama Liwale na wengine wanazungumza Nanyumbu kwamba iwe katika sehemu ya Mkoa mpya wa Selous.

Katika majadiliano yaliyofanyika, maeneo hayo hayakutajwa kwamba ni sehemu ya mapendekezo ya Mkoa mpya. Sasa kwa sababu ni mapya basi naomba sana Mheshimiwa Kuchauka ayapeleke kwenye Mkoa wake wa Mtwara ili waweze kuyajadili kuanzia huko. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Munde.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa MwenyeKITI, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa MwenyeKITI, kabla sijaanza kuuliza swali, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kugawa *tablets* kwa walimu wakuu wa shule za msingi ili kuboresha elimu na ufundishaji. Mheshimiwa Rais aliahidi na ameanza kutekeleza, angalau ni kawaida yake kuahidi na kutekeleza, tunampongeza sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa MwenyeKITI, kwa kuwa taratibu zote za kuugawa Mkoa wa Tabora zilishakamilika na Serikali iliahidi kutimiza kuugawa mkoa huo ambao una Wilaya saba na una wakazi wengi na kuwasababishia wakazi wa mkoa huo kukosa huduma za msingi kama inavyostahili.

Je, ni lini sasa Serikali itaugawa Mkoa Tabora kama ilivyogawa Mkoa wa Mbeya kuwa Songwe na kama ilivyogawa Shinyanga na Simiyu ili wananchi wa Tabora nao waweze kupata haki zao za msingi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe maelezo kwamba sisi katika Mkoa wa Tabora tunajivunia sana utendaji kazi wa Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah kwa jinsi ambavyo anafuatilia masuala mbalimbali kwenye Mkoa wa Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipotembelea Mkoa wa Tabora mwaka 2017 na kufanya mkutano wa hadhara pale Nzega lilitokeza swali hili la ombi la kuugawa Mkoa wa Tabora kwamba tuwe na Mkoa mpya wa Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yake katika mkutano ule ndio ambayo yamejenga mwongozo wa kitaifa kwa sasa kwamba kuna haja kwanza kuimairisha miundombinu na mahitaji mengine katika Mikoa, Wilaya na Halmashauri mpya ambazo zilishaanzishwa tangu zamani ili tukikamilisha uimarishaji huo ndio tuje kwenye mikoa mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mkoa wa Nzega limeshajadiliwa *RCC* na vikao vyote vimekamilika, tutakapokuwa tumeimarisha maeneo haya mapya yaliyopo, Mkoa huo mpya wa Nzega, naomba sana watu wa Nzega wasiendelee kubishana tena, utatangazwa mara moja na utapewa kipaumbele.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum.

**Mkakati wa Serikali Kufanya Utumishi wa
Umma Uwe wa Kuaminika**

MHE. RUTH H. MOLLEL aliuliza:-

Utumishi wa umma ndiyo injini ya maendeleo katika nchi. Watumishi wa umma hawatakiwi kuwa na mrengo wowote wa itikadi ya kisiasa ili kutumikia wananchi kwa muda wote hata yanapotokea mabadiliko ya vyama tawala baada ya uchaguzi.

(a) Je, Serikali ya Awamu ya Tano ina mkakati gani wa kuhakikisha utumishi wa umma ni thabiti na wa kuaminika wakati wote?

(b) Je, ni watumishi wangapi wa umma ambao wamegombea vyeo katika chama tawala wakati wapo katika ajira ya utumishi wa umma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Katibu Mkuu Mstaafu, *senior citizen* mwenzangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 65(1), Jedwali la Tatu, Sehemu ya IX ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 ikisomwa kwa pamoja na aya ya 50 ya Taratibu za Uendeshaji Utumishi wa Umma za mwaka 2003, watumishi wa umma wanatakiwa kutokuwa na mrengo wowote wa itikadi ya siasa ili kuwatumikia wananchi kwa muda wote bila ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa kanuni hizi zimeendelea kuwepo pia katika Serikali ya Awamu ya Tano na hivyo kuendelea kuimarisha utumishi wa umma.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa mwaka 2015 unaosimamia ushiriki wa watumishi wa umma katika uongozi wa kisiasa watumishi wote wa umma waligombea na kupata nafasi za uongozi wa kisiasa walistaafu na hawapo tena katika utumishi wa umma.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wameteuliwa wengi wao walikuwa ni wana-CCM walioshindwa katika kura za maoni, nao ndio wasimamizi wa uchaguzi. Kuna wengine hata kwa mfano huyo wa Ubungo mpaka leo anahudhuria vikao vya CCM.

Swali langu, ikiwa tutaleta orodha ya Wakurugenzi ambao tunajua ni wana-CCM na walikuwa katika kura za maoni; je, Serikali itakuwa tayari kuwaondoa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; tunao Wakuu wa Mikoa ambao wanalipwa kwa pesa za walipa kodi, Watanzania wenye vyama na wasiokuwa na vyama, lakini wengi wameonesha itikadi za mrengo wa kisiasa; tukiangalia Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mkuu Mkoa wa Manyara na wengine; je, Serikali ina kauli gani kuhusu hilo? Ahsante. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Kama wewe.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Yeye alikuwa Katibu Mkuu huyo na ni mtumishi. Yeye mbona...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawasihi sana, tuache ushabiki. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kumpongeza Waziri Kivuli wa Wizara yangu, mdogo wangu Mheshimiwa Ruth Mollel kwa jinsi anavyofuutilia utendaji kazi wa Wizara yangu na hiyo ndiyo kazi ya Waziri Kivuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi ye yote utakayemchagua katika nchi hii lazima kuna chama anachokipenda. Huyu yuko pale baada ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi na Waraka ule wa Utumishi wa Umma unasema; "Mtumishi wa umma anayeteuliwa na Rais, endapo hataridhia kufanya ile kazi, ana ruhusa ya kumwambia Mheshimiwa Rais, naomba niendelee na kazi yangu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa Wakurugenzi walipokuwa wanafanya kazi, wameshakoma kazi waliyokuwa wanaifanya, kazi iliyobaki sasa hivi ni Mkurugenzi wa Halmashauri. Nataka niseme nchi zote duniani baada ya uchaguzi, Rais anayeingia madarakani, anapanga safu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Marekani, *State House* yote, wahudumu, wafagizi wote, akiingia Rais mpya, anaondoa anapanga watu wake. Sasa kama Mheshimiwa Rais kafanya hivyo kwa hao Wakurugenzi, ndivyo alivyoona inafaa, nasi ndani ya Serikali, tunaona wanachapa kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule wa Ubungo kuhudhuria vikao, nataka niseme hivi, mkishakuwa na chama tawala, siku zote wajibu wenu ni kuihaji Serikali. Mkurugenzi wa Ubungo sio Mjumbe katika vikao vya CCM, lakini anaweza kuitwa saa yoyote aende kuelezea utekelezaji wa llani ya Uchaguzi katika Jimbo la Ubungo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kuhusu Wakuu wa Mikoa; kauli gani Wakuu wa Mikoa wanaoshiriki siasa, wanaaoonesha wanapendelea upande mmoja, nataka niseme hivi, Mkuu wa Mkoa ndio mwakilishi wa Rais katika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wilaya ile. Mkuu wa Mkoaa ndio Rais wa Mkoaa ule. Rais ni neno la kiarabu, maana yake kichwa. Kwa hiyo, kichwa cha Mkoaa ule ni Mkuu wa Mkoaa. Huyu Mkuu wa Mkoaa anamwakilisha Rais. Hutegemei huyu Mkuu wa Mkoaa afanye mambo tofauti na anavyofanya Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kusema kwamba nchi hii tuna chombo kinaitwa Mahakama. Mhimili wa Mahakama kazi yake ni kutafsiri sheria. Pale mtu ameona kwamba amekuwa *aggrieved*, au pale mtu ameona kwamba ametendewa ndivyo sivyo, basi tufuate mkondo wa sheria. Baadhi yao mnaowasema, walikuja hapa kwenye maadili, wakasikiliza, wakawa *cleared*, wakaonekana hawana makosa. (*Makofi*)

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mkuchika wewe mtaalam.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na baada ya maeleo ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Tanzania ni nchi ya Mfumo wa Vyama Vingi na kwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ndio Msimamizi wa Uchaguzi.

Je, Serikali sasa iko tayari kuleta mabadiliko ya Sheria ya Mkurugenzi wa Halmashauri asiwe msimamizi wa uchaguzi hasa kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019?
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopo sasa, zilizotungwa na Bunge hili

zinasema Mkurugenzi wa Halmashauri, Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa unapofika wakati wa uchaguzi ndiyo msimamizi wa uchaguzi. Pale inapotokea kwamba Bunge hili litaona haja ya kubadili, hoja iletwe, tutaijadili. Ikibadilishwa, mimi mtumishi wa Bwana nitatenda kama Bwana anavyotaka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa Waitara.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba nianze kwa kuwapongeza Wakurugenzi wote nchini akiwemo Kayombo wa Ubungo na Arusha Mjini kwa kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa kuwa ili kuwa thabiti katika utumishi wa umma ni pamoja na kuwajali watumishi; na Mheshimiwa Rais alianza kuonyesha mfano kwa kuwajali walimu wa shule za msingi kwa kuwapatia *tablets*, napenda kufahamu, je, Serikali ina mikakati gani kuwajali watumishi wa umma katika maslahi yao? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua Serikali inafanyaje katika kuwajali watumishi. Tarehe 1 Mei, 2018 Mheshimiwa Rais alipohutubia Uwanja wa Samora pale Iringa alipokuwa mgeni rasmi, alipokuwa anajibu risala ya wafanyakazi alisema; Serikali yake inatumia fedha kadri zinavyokusanywa. Kwa hiyo, ataboresha maslahi ya watumishi wa umma kulingana na uwezo wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alisema; "mimi sitangoja *May Day*, siku yoyote nitakapotosheka kwamba hali ya Mfuko

wa Serikali inaniruhusu kufanya nyongeza, kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma nitafanya hivyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kwamba Serikali inawajali watumishi, inawapeleka mafunzo, wanapewa mikopo, wengine tunawadhamini katika kupewa mikopo, tunawapeleka kusoma nchi za nje katika taaluma mbalimbali, hiyo yote ni kujali watumishi, maana kumjali mtumishi siyo lazima kumpatia fedha tu, hata ukimpeleka mafunzo, unamjali mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo yote niseme kwa kifupi kwamba tunaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma, lakini kwa upande wa mishahara kama nilivyosema tutapandisha mishahara pale hali ya nchi itakaporuhusu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kauli ambayo Wakurugenzi walielezwa kwamba wamepewa ajira, wamepewa magari na wanalipwa mshahara na Mheshimiwa Rais, ole wake Mkurugenzi ambaye atamtangaza mpinzani. Kauli hii imeleta sintofahamu, kutojiamini na hofu katika chaguzi mbalimbali. Nini kauli ya Serikali sasa juu ya kauli hii ya tishio la uchaguzi ulio huru na hakii? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ndugu yangu Mheshimiwa Waitara hajalieleza Bunge hili kwamba kauli hiyo imetoka lini? Alisema nani? Katika shughuli gani?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mzee wa zamani, nilifundishwa kwamba *government moves on paper*. Kwa hiyo, huwezi ukaja Bungeni hapa ukasema fulani alisema hivi na hivi na hivi. Kwa kifupi tu nataka nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Waitara kwamba Wakurugenzi tumewafundisha na tumewafanyisha semina wafanye kazi kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki.

Na. 399

Ripoti za CAG za Ufanisi Kutofanyiwa Kazi

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Kwa kuwa Ripoti za Ukaguzi za Ufanisi unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeonesha kuna mapendekezo yanayotolewa baada ya ukaguzi mengi hayafanyiwi kazi na kwamba upungufu unaoibuliwa hujirudia mwaka hadi mwaka.

(a) Je, Serikali inakubaliana na pendekezo la kuanzisha kitengo maalum kitakachoratibu utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za ufanisi?

(b) Je, Serikali inakubaliana na pendekezo kuwa baada ya Kamati ya PAC kujadili taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi ipeleke maoni yao kwa Kamati za Kisika ili kutoa fursa kwa Kamati hizo kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mapendekezo ya CAG hasa katika maeneo ya kisera na kiutendaji kwa mujibu wa Kanuni za Bunge?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa ufanisi wa miradi unaratibiwa na kufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye hutoa mapendekezo yanayohitajika kutelekelezwa na wakaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya taarifa ya kaguzi za ufanisi kukamilika, huwasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana na sekta husika, mfano Kilimo, Elimu, Maji na kadhalika, tofauti na ilivyo kwa taarifa za Ukaguzi wa Serikali Kuu na mashirika ya umma, ambapo taarifa zake huwasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha na taarifa ya kaguzi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa za ufanisi (*performance audit*) huratibiwa na Wizara husika. Wizara za kisekta ndizo ambazo hufuatilia na kuhakikisha kuwa mapendekezo ya *CAG* yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maeleo haya, haitakuwa vyema kuanzisha kitengo maalum cha kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kwani kwa kufanya hivyo ni kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali. Hata hivyo Wizara, Idara au taasisi zinatakiwa kuwa na mpango kazi wa kuhakikisha kuwa mapendekezo yanayotolewa na *CAG* kupitia taarifa hizo, yanatekelezwa ipasavyo. Aidha, kupitia taarifa hizo za ufanisi, kunakuwa na masuala ambayo utekelezaji wake ni wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali siku zote ipo tayari na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni zilizowekwa zikiwemo Kanuni za Bunge. Hata hivyo, Serikali haina mamlaka ya kupanga au kuingilia majukumu yanayopaswa kutelekezwa na Kamati za Kudumu za Kisekta za Bunge. Hivyo basi, Bunge lako tukufu lina nafasi ya kuamua juu mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya *CAG* iliyoishia Juni, 2017 imeonesha kwamba katika kaguzi zilizofanywa hasa katika Shirika la *RAHCO* ilitumia shilingi bilioni 20 kufanya upembuzi yakinifu wa miradi minne, lakini shilingi bilioni 20 zimepotea kutokana na kwamba miradi hiyo haikutekelezwa au haitekelezeki.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kuna harufu ya ujisadi katika miradi hii minne ambayo ametumia shilingi bilioni 20 wakati ikijulikana miradi hii haiwezi kufanya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, imeonekana Wabunge wengi walikuwa wamelalamikia miradi ambayo inafanywa chini ya viwango ikitekelezwa na Wizara za Maji na Wizara za Ujenzi hasa *TANROADS* na kwamba pesa nyingi inatumika kwenye upembuzi yakinifu lakini nakuta miradi hiyo haifanywi.

Je, Serikali inakubaliana nami kwamba kuna sababu ya kumwomba Mheshimiwa Spika aunde Tume ya Kibunge ambayo itachunguza haya yote kwamba inakuwaje ifanywe miradi ya upembuzi yakinifu, lakini miradi hiyo haitengewi hela mwaka hadi mwaka? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza kwamba kwenye upembuzi yakinifu wa *NAFCO* kwamba kulikuwa na ujisadi. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba hizi ni taarifa za kisekta na zinafanyiwa kazi na Wizara husika

za kisekta. Inakuwa ni ngumu kwa mimi kusema kulikuwa na harufu ya ujisadi kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amelitamka hili ndani ya Bunge lako tukufu; Serikali yetu ni moja, tunalifanyia kazi kuona jambo hili linafanyiwa kazi kabla ya kukiri aidha kulikuwa na ujisadi au hakukuwa na ujisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, nimesema kwenye jibu langu la msingi Serikali yetu hufuata Katiba, Sheria, Kanuni zikiwemo Kanuni za Bunge lako tukufu na hivyo Serikali haina mamlaka ya kulipangia Bunge nini cha kufanya. Kama Bunge lako tukufu litajiridhisha kuna umuhimu wa kuunda Tume kwa ajili ya kazi hiyo anayopendekeza Mheshimiwa Mbunge, Serikali yetu iko tayari kabisa kuona hilo linatekelezwa kwa sababu ni majukumu ya Bunge kusimamia Serikali yetu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Haya Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali wakati ikitoa ufanuzi kuhusiana na kukosekana kwa taarifa za matumizi ya shilingi trilioni 1.5 ilielezwa kwamba kati ya fedha zile shilingi bilioni 200 ni makusanyo ya Zanzibar.

Sasa Mheshimiwa Waziri kabla nazo hazijatumbukia katika kero ya Muungano ni lini fedha hizi zitafika Zanzibar? (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo la uchokozi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili liliulizwa wakati tukijadili bajeti ya Wizara yetu ya Fedha na Mipango na sisi kama Serikali tuliamu kulijibu makusudi kwa sababu tunafahamu mchakato wa kujadili hoja hizi za CAG ukoje, itakapokwenda kwenye Kamati ya PAC tukija hapa itajadiliwa kwa kina. Hata hivyo, naomba kusema yafuatayo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 203 ni fedha inayokusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania Zanzibar na huwa hazivuki maji kuja Tanzania Bara. Zinakusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuingia moja kwa moja kwenye akaunti.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Naomba msikilize basi niwape elimu ili tuweze kuelewana. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo hukusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania inayofanya kazi zake Zanzibar; na zinapokusanya fedha hizo zinasomeka kwenye *financial statement* za Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa sababu zinakusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Fedha hizo hazivuki maji kuja Tanzania Bara, huingia moja kwa moja kwenye akaunti kuu ya *Pay Master General Zanzibar*. Kwa hiyo, fedha hizo zimekwenda moja kwa moja kwenye akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ya Zanzibar. *(Makof)*

MWENYEKITI: Hayo ndio maelezo sahihi. Tunaendelea na swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini na linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Na. 400

**Kusaidia Maeneo Yaliyoathiriwa na Ujio wa
Wakimbizi - Kigoma**

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE (K.n.y. MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO) aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma hususan Wilaya za Kasulu na Kibondo zimekuwa makazi ya wakimbizi kwa muda mrefu sana.

Je, ni lini Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na *UNHCR* itakuja na mpango kabambe wa kusaidia maeneo yaliyoathiriwa na ujio wa wakimbizi hao (*a comprehensive plan and support for refugee affected areas*)?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya maeneo ambayo hupokea wakimbizi nichini hupata athari mbalimbali ikiwemo uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (*UNHCR*) inatekeleza mipango mbalimbali inayolenga kuboresha huduma kwenye jamii katika Wilaya zinazohifadhi wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya za Kibondo na Kasulu huduma ambazo zimekuwa zikiboreshwa ni pamoja na afya, elimu, kilimo, masoko, ujasiriamali pamoja na hifadhi ya mazingira.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sijaridhika sana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na athari kubwa sana zilizoletwa na ujio wa wakimbizi Mkoani Kigoma, ongezeko la watu, miundombinu isiyotosheleza, ni lini hasa mpango kabambe utaletwa? Naomba *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ujio wa wakimbizi ndani ya Mkoa wa Kigoma, Makambi ya Wakimbizi ya Kibondo, Kasulu na Kakonko yamesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira; je, Serikali inalijua hilo? Ni mikakati gani ya Serikali katika kusaidia Mkoa wa Kigoma kutokana na athari hizo?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu maswali mawili tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza naona halijawa wazi zaidi, lakini kwa niliviyolelewa, ameuliza kuna mpango gani kabambe? Nadhani alikusudia mipango ambayo Serikali inafanya kwa kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa katika kuhakikisha kwamba shughuli na huduma za maendeleo katika jamii, wananchi ambao wanazunguka makambi yale wanafaidika. Kama hivyo ndiyo, basi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna miradi mingi ambayo imeshatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali na mashirika haya ya kimataifa chini ya *UNHCR* katika kuboresha huduma za jamii katika maeneo husika, kama ambavyo nimezungumza katika sekta ya afya, masoko, maji, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na mazingira, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ujio wa wakimbizi katika Mkoa wa Kigoma kwenye makambi yetu umeleta athari kwenye eneo la mazingira. Kwa kutambua hilo, ndiyo maana Serikali imechukua jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kwamba inakabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika mambo ambayo tumefanya, kwanza ni matumizi ya majiko ambayo wanaita majiko ya ubunifu, ambayo sasa hivi badala ya kutumia kuni kukata miti ovyo, aina ya upikaji na uandaaji wa chakula kwa wakimbizi umebadilika kwa kutumia teknolojia ambazo zinapunguza athari kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika ukataji miti ambapo fito zilikuwa zikitumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, umepungua kwa kiasi kikubwa. Sasa hivi nyumba ambazo zinajengwa ni za kudumu kwa kutumia matofali, pamoja na kutoa elimu kwa wakimbizi na jamii husika juu ya umuhimu wa kuweza kudhibiti mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ni miongoni mwa mambo ambayo Serikali imekuwa ikifanya kuhakikisha kwamba athari ya mazingira inapatiwa ufumbuzi katika maeneo hayo ambayo yana makambi ya wakimbizi.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, linaloulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwamoto.

Na. 401

Sheria ya Michezo ya Mwaka 1967

MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO) aliuliza:-

Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha maendeleo ya michezo mbalimbali lakini sheria inayosimamia michezo ya mwaka 1967 ina upungufu makubwa sana.

(a) Je, kwa nini Serikali haijatunga sheria mpya ya michezo ambayo itakwenda sambamba na mahitaji ya jamii kwa sasa?

(b) Je, kwa nini Serikali haina bajeti kwa ajili ya Timu za Taifa zinazobeba bendera kwa ajili ya kuitangaza nchi Kimataifa?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
aliuju:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba kwa ridhaa yako kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro nitoe pongezi kwa Mabingwa wa Ligi ya Tanzania Bara Simba, kwa kufanikiwa kutinga fainali ya michuano ya *Sport Pesa Super Cup* nchini Kenya. Simba wamethibitisha kuwa hawakupata ubingwa wa Tanzania Bara kwa kubahatisha, bali kwa soka la viwango na sasa wanaingia fainali kupambana na mabingwa wa Kenya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko katika hatua za mwisho kabisa kukamilisha maboresho ya sera ya michezo ya mwaka 1995 na sera mpya tutakayoipitisha ndani ya mwaka huu, itakuwa msingi wa sheria mpya ya michezo nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya michezo nchini ambayo inaendana na ukubwa wa mashindano yanayotukabili. Kwa mfano, mwakani Tanzania ni mwenyeji wa mashindano ya *AFCON* ya mpira wa miguu kwa vijana chini ya umri wa miaka 17. Hivyo, mbali na vyanzo vingine vya fedha, Bunge hili tukutu limeidhinisha shilingi billioni moja itumike kuboresha miundombinu ya Kiwanja cha Taifa na Kiwanja cha Uhuru na shilingi 293,619,000 kwa maandalizi mengine yanayohusiana na *AFCON*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utatuzi wa migogoro katika sekta ya michezo bado ni changamoto kubwa sana; je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuanzisha

chombo ambacho kitakuwa chini ya BMT ili kuweza kusaidia kutatua migogoro badala ya kuacha watu wanaenda mpaka FIA kwenda kufuata haki zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inasisitiza suala la uimarishaji na ujenzi wa viwanda na michezo ni moja ya kiwanda kikubwa; je, Serikali sasa itakuwa tayari kuandaa kongamano la Waheshimiwa Wabunge wanamichezo na wadau ili kujitathmini tulikotoka, tulipo na tunakokwenda?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mpaka sasa sijaona kama utaratibu tuliuweka chini ya Baraza la Michezo Tanzania na chini ya Mashirikisho yanayohusika ya michezo kwamba umeshindikana kiasi cha kuunda chombo kingine kipyga. Sisi kama Wizara tuko tayari kupokea maoni kutoka kwa wanamichezo kama Mheshimiwa Mwamoto, tuweze kuelewa umuhimu wa kuunda chombo kipyga sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu kuandaa kongamano, namwomba Mheshimiwa Mwamoto, ye ye mwenyewe anaweza kuanzisha hilo, na sisi tutamuunga mkono kwa sababu suala la kongamano ni kujadiliana tuweze kusonga mbele katika michezo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sima.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ligi yetu ya Tanzania imekuwa ikitumia gharama kubwa sana hata kwenye usajili wa zaidi ya shilingi bilioni moja kwenye timu kadhaa, lakini wanaenda kupokea shilingi milioni 86 na wamecheza kwa mwaka mzima.

Je, Serikali ina mkakati gani kuifanya ligi hii ya Tanzania kuwa ina ushindani? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Sima kuhusu usajili na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimweleze Mheshimiwa Sima kwamba sisi kama Wizara bado hatujaona tatizo la usajili na ushindani katika ligi, lakini kama ni matumizi ya pesa, kwa kweli soka la leo ni la pesa. Usipokuwa na pesa, huwezi kabisa ukaendesha mchezo wowote wa mpira. Ndiyo maana unawenza kuona maendeleo mazuri ya timu kama *Singida United*, nao naomba niwapongeze kwa kazi nzuri ambayo wameifanya Kenya na tuwaombee kama ambavyo tunawaombea Simba waweze kufanya vizuri wawe washindi wa tatu katika mashindano ya Kenya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Michezo ni pamoja na viwanja. Naipongeza sana Serikali kwamba tuna uwanja mzuri sana, Uwanja wa Taifa, lakini uwanja ule kwenye eneo la VIP na juzi wananchi wote na Mheshimiwa Rais walikwenda pale kushuhudia mechii ya Simba na mechii ya Kagera. Eneo lile halina kibanda au kinga ya juu au mvua wakati hali ya hewa inabadilika.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha kuwa eneo lile sasa linawekewa kibanda maalum kuzuia mvua kwa watazamaji wa kawaida na viongozi wa Kitaifa watakapokwenda kutazama mpira?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hili Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba

kuna upungufu katika Uwanja wetu wa Taifa na ndiyo maana tulipokuja mbele ya Bunge lako tukufu kuomba tutengewe pesa kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Taifa, hiyo ni moja ya upungufu ambao utatatuliwa kwa pesa ambayo tumeiomba na ambayo inakidhi viwango vya CAF na FIFA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata walipokuja juzi, tulipowaeleza kwamba matarajio yetu ni kutumia hiyo shilingi bilioni moja kwa ajili ya marekebisho ya aina hiyo katika Uwanja wa Taifa, walitukubalia. Kwa hiyo, mabadiliko kama hayo tuyategemee katika Uwanja wa Taifa katika muda sio mrefu kutoka sasa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wizara na Baraza la Michezo zimekuwa zikiweka nguvu katika kuushughulikia mchezo mmoja tu wa mpira wa miguu na kusahau michezo mingine na ndiyo maana hata wakati uwanja mkubwa wa Taifa unajengwa, tuliambiwa kwamba inajengwa *sports centre*, lakini imejengwa *football ground*. Kwa maana hiyo, wenyewe michezo mingine wanashindwa kutumia miundombinu hiyo. (*Makofii*)

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutenga ukumbi mmoja kati ya kumbi zilizokuwa kwenye Uwanja wa Taifa kuwa *Boxing Academy* ili wacheza ngumi na wenyewe waweze kupata sehemu ya kufanya michezo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna jumla ya michezo 38 iliyosajiliwa hapa nchini na tuna michezo mipya kabisa tisa ambayo mingine nikiitaja hapa wengine hatuwezi kuilewaa. Kwa hiyo, kutokana na hiyo, sisi Kiwizara tunapanga mipango yetu kwa mahitaji na jinsi ambavyo michezo yenye kifaa kuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba kuna mchezo mwingine tunaupendelea, hapana, ni kutokana na wadau wenyewe.

Kwa mfano, leo hii hatuwezi tukasema tuweke katika mipango yetu namna ya kuendelea na mchezo wa *freese B* ambaao ni mchezo wa kisahani umeingia nchi, kuna mchezo wa kabadi, kuna mchezo wa kengele (*goal ball*), kuna mchezo wa *roll ball*, kuna mchezo wa *wood ball*; sasa hiyo michezo tunawategemea wadau mwiendeleze ifikie kiwango ambacho tunasema tunaweza kuwa na ushindani katika nchi hii na tukaweza kuifanyia utaratibu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Mtolea ni zuri kwamba tuna maeneo makubwa sana Uwanja wa Taifa, lakini pale penye mahitaji, wadau wenyewe waeleze na sisi tunaweza kutoa maeneo hayo kuweza kuyaendeleza kwa michezo mingine.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shangazi. Swalil la nyongeza Shangazi. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Saleh Ally. (*Kicheko*)

Na. 402

Umuhimu wa Mchezo wa *Chess Nchini*

MHE. ALLY SALEH ALLY aliuliza:-

Mchezo wa *chess* au sataranji unakuza akili, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi na ni mzuri sana kwa vijana ambaao wanakulia na kuingia hasa katika masomo ya sayansi na ufundi.

(a) Je, mchezo huo umejikita kiasi gani hapa nchini hadi sasa?

(b) Je, kunaweza kuwa na mipango ya kufanya juu ya mchezo huo kuwa wa lazima na sehemu ya mtaala kwa kuiga hasa nchi za Ulaya ya Mashariki?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Ally Saleh Ally kama ilivyo kwa michezo mingine, mchezo wa *chess* au saratanji unakuza akili, hilo tunakubali, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi. Hata hivyo, mchezo huu bado haujaenea sana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhamasisha kuwa michezo ikiwemo mchezo wa *chess* inaimarika nchini. Wizara, kupitia Baraza la Michezo la Taifa na Chuo cha Maendeleo ya Michezo - Malya kwa kushirikiana na wadau wa mchezo huu itaangalia uwezekano wa kutoa mafunzo kwa lengo la kuueneza mchezo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha wananchi katika maeneo mbalimbali kushiriki katika mchezo huu kama inavyofanya katika michezo mingine ili kuueneza mchezo huu kwa manufaa ya jamii kwa ujumla, kwani tayari umeshasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuufanya mchezo huu kuwa wa lazima kufundishwa kwenye shule kwa kuingiza kwenye mitaala yetu. Pia suala la kuingiza mchezo kuwa sehemu ya mtaala linahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara mbalimbali na hasa baada ya kujiridhisha kwa kufanya tafiti za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, Waheshimiwa Wabunge na wadau wote wa Sekta ya Michezo waendelee kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha kuwa michezo, ikiwemo mchezo wa *chess* inasonga mbele. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ally Saleh Ally.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mchezo wa *chess* unachezwa na karibu watu milioni 800 duniani kote, lakini pia katika hali ya ushindani wa hali ya juu unachezwa na karibu watu milioni 20. Pia kuna *chess olympia* yaani *olympic* ya *chess* peke yake. Kwa jibu hili la Serikali, sioni nia yao kama wanataka mchezo huu ukue ufikie katika huo ukubwa (*magnitude*) ambayo nimeielezea kwa sababu wanasesma kwamba ukuzwe na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari; kwa sababu mchezo huu hauna gharama kubwa katika kuuwekeza, ipo tayari kuwashawishi *Cooperate Tanzania* iuchukue mchezo huu, ikuze na uweze kuchezwa katika upana mkubwa angalau tuwakute wenzenzu Kenya, Uganda na Zambia majirani zetu ambao wapo mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mchezo huu unakuza akili na ufikiri, lakini mchezo huu maumbile yake unafundisha namna ya kujihami na namna ya mbinu za kijeshi. Je, Serikali iko tayari kutumia nafasi yake kuona kwamba mchezo huu unachezwa katika hali ya kukuza vyombo vyya ulinzi? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba tu nisisitize kama nilivyo sema kwenye swali langu la msingi kwamba kwa kweli hakuna mchezo wowote hapa nchini uliokuzwa na Serikali bila wadau, haitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Ally Saleh ajitahidi kwa nafasi yake ya Ubunge kuhimiza wadau mbalimbali waweze kuubeba huu mchezo kama michezo mingine inavyofanyika na Serikali tupo tayari

kutengeneza miundombinu sahihi na mazingira ya kuweza kuhakikisha kwamba mchezo huu unakua kwa kasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchezo wa *chess* ni kweli kabisa nakubaliana naye kwamba ni mchezo ambao unahitaji akili, kama vilevile ambavyo mchezo wetu wa utamaduni wa bao unavyohitaji akili katika kuuchenza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nimefurahi sana wadau wa bao wameamua sasa huu mchezo uende Kitaifa. Nampongeza sana mwanabao mashughuli hapa nchini Mandei Likwepa na wenzake waendelee na sisi tutawasaidia kuweza kuuhamasisha huu mchezo ambao ndiyo *chess* ya Kiafrika. Nina uhakika tukiuongezea vilevile manjonjo mbalimbali unaweza kuwa pengine bora kupita hata huo wa *chess* kwa sababu hatujaufanya kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie tu kwa kusema kwamba tunakubali mchezo wa *chess* ni muhimu, ni mkubwa na unahitaji akili hata kwa majeshi ungefaa sana, lakini hata kwa wanafunzi wetu kutoka shule ya msingi mpaka Vyuo Vikuu unafaa sana, lakini naomba wadau wawe mstari wa mbele badala ya kuisubiri Serikali ndiyo itangulie mbele katika mchezo huu.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 403

**Serikali Kutangaza Vivutio vya Utalii
katika Mkoa wa Iringa**

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Serikali inafanya mkakati gani ili kutangaza vivutio vilivyopo katika Mkoa wa Iringa katika sekta ya utalii?

Je, Serikali inavitambua vivutio hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa yenye vivutio vingi vya utalii kama vile Hifadhi za Taifa za Ruaha na Udzungwa, Makumbusho ya Mtwa Mkwawa ya Kalenga, Isimila, Eneo la Zana za Mwanzo za Mawe na Maumbile Asilia na Makumbusho ya Mkoa ambayo inaonesha utamaduni wa asili wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 na mpango kabambe wa uendelezaji utalii, Serikali imekuwa ikitangaza vivutio vya utalii vilivypopo katika maeneo mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Iringa. Mpango kabambe wa kuendeleza utalii nchini ulioandaliwa mwaka 1996 na kufanyiwa mapitio mwaka 2002 umeainisha Mkoa wa Iringa kama kitovu cha maendeleo ya utalii (*tourism hub*) kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuainisha vivutio katika Mkoa wa Iringa lilianza kufanyika mwaka 2007 ambapo mpaka sasa takribani maeneo 38 ambayo ni vivutio vya utalii yameainishwa katika Wilaya za Mufindi, Kilolo na Iringa. Kazi inayofuata sasa ni kuendeleza na kutangaza vivutio hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia taasisi zake ikiwemo Bodi ya Utalii Tanzania imeweka mikakati madhubuti ya kutangaza utalii. Mikakati hii ni pamoja na kujenga utambulisho wa Tanzania (*Destination Tanzania Brand*), kukuza maonesho ya utalii wa Kimataifa yanayofanyika ndani na nje ya nchi kama vile Karibu Kusini, kuanzisha *channel* ya utalii, kuanzisha Studio ya kutangaza utalii kwa njia ya TEHAMA, kuadhimisha Mwezi wa Urithi (*Urithi Festival*) na kuimarisha uhamasishaji kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwemo wanafunzi. Vivutio vya utalii katika Mkoa wa

Iringa vimejumuishwa katika mikakati hii ya kutangaza utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo hapo juu na ili utalii Mkoani Iringa, Serikali imeendesha mafunzo ya muda mfupi ya utalii na ukarimu kuititia mradi wa *SPANEST* kwa takribani watu 300, imefungua Ofisi ya Utalii ya Kanda ya Kusini iliyoko Iringa na imezindua mradi wa kukuza utalii Ukanda wa Kusini ujulikanao kama *REGROW*. Aidha, Iringa ni mionganoni mwa mikoa iliyoajiri Maafisa Utalii kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Halmashauri za Wilaya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza. Kwanza kabisa nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo amenipatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imefungua mradi wa *REGROW* ambao utafanya kazi ya kukuza utalii wa ukanda wa Kusini ukiwemo Mkoa wa Iringa; je, Serikali ina mkakati gani wa kujengea uwezo wananchi walipo katika mkoa wetu ili watumie vizuri fursa hiyo kujiajiri na kuweza kujipatia kipato? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nje ya maeneo ya utalii kuna historia kubwa za machifu akiwemo Mtwa Mkwawa, lakini kuna Kituo cha Kalenga, eneo la Mlambati ambapo Mwalimu Nyerere aliweka jiwe la msingi mwaka 1998 kama ukumbusho wa miaka mia moja.

Je, ni lini Serikali itachukua ya kuyaboresha kwa ajili ya kuvutia watalii na kuhakikisha kwamba pesa inayopatikana katika maeneo hayo, inawasaidia wananchi wanaozunguka eneo hilo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kabla sijajibu haya maswali nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza kwa jinsi ambavyo amesimama imara katika kuupigania Mkoa wa Iringa, lakini pia alipigania sana kuhakikisha kwamba Kituo cha Utalii kinajengwa pale Kihesa, Kilolo. Kwa kweli nampongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake ameuliza; je, tuna utaratibu gani wa kuhakikisha tunawajengea uwezo? Naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba katika mradi mkubwa ambao tunaenda kuutekeleza Mikoa ya Kusini unaohusu hifadhi nne yaani Udzungwa, Mikumi, Ruaha pamoja na Selous ya Kaskazini, tuna utaratibu wa kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi wa Mkoa wa Iringa waweze kufaidika na huu mradi, ni lazima wajengewe uwezo ili waelewe umuhimu wa kuuendeleza utalii na wawe tayari kuwakarimu watalii watakaokuwa wanatembelea katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi sasa tuna mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba, kwanza tunawaelimisha namna ya kuanzisha makampuni ya kitalii ya kuongoza watalii, lakini pili, namna watakavyowakarimu pamoja na kuwaonyesha mambo mbalimbali ambayo yapo katika Mkoa wa Iringa ukiwemo utamaduni wa Iringa na tatu, ni pamoja na kuwapokea na kuwakarimu katika hoteli mbalimbali. Kwa hiyo, hii mipango yote tutaitekeleza katika mwaka wa fedha huu unaoanza Julai. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal i la pili kuhusu kile Kituo cha Kalenga, kama alivyosema kweli kabisa miundombinu bado haitoshelezi. Hivi sasa tuna mpango kabambe wa kuhakikisha barabara ya lami inajengwa kutoka Iringa hadi kwenye Iango kuu la Ruaha. Wakati tutakapokuwa tunajenga ile barabara, tutaangalia uwezekano wa kuimarisha ile miundombinu, kuchepusha pale kupeleka

katika hiki Kituo cha Kalenga kwa sababu ni karibu ili tuhakikishe kwamba nako panafikika kiurahisi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ehe, naanza na Mheshimiwa Atupele Mwakibete. (*Makofi*)

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Mbeya una vivutio vya asili kama ulivyo Mkao wa Iringa na vivutio hivyo vya asili ni kama Mlima Rungwe, Mlima Kejo, Ziwa Nyasa na maeneo mengine kama Maziwa ya Masoko, Kingururu, Iramba pamoja na Daraja la Mungu.

Je, Serikali ina mpango gani kuvitangaza vivutio hivi ili wananchi wanaoishi maeneo hayo waone umuhimu wa uwepo wa vivutio hivyo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa Mkao wa Mbeya una vivutio vingi sana kama ulivyo Mkao wa Iringa na kama ilivyo mikoa mingi. Hivi sasa kama nilivyosema, tunayo mikakati kabambe ya kuhakikisha kwamba vivutio vyote nchi nzima vinatangazwa. Nimesema tutaanzisha *studio* ya kutangaza na tutaanzisha *channel* ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mikakati hii, maeneo yote yenye vivutio vya utalii Mkao wa Mbeya nayo yataingizwa katika huo mpango kabambe wa kutangaza ili kusudi watalii mbalimbali waweze kujua Tanzania na Mkao wa Mbeya kuna nini? Nina uhakika Mheshimiwa Mbunge atafaidika sana hasa baada ya kuanza kutangaza maeneo haya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Mlata ajiandae.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Mkao wa Mtwara una vituo vingi sana vya kitalii, kwa mfano, ile *beach* ya Msimbati ambayo inaweza kuendesha gari, kuna Shimo la Mungu kule Newala, lakini vilevile Newala kuna Kituo cha Utamaduni wa Kimakonde na Mji maarufu wa asili Mikindani.

Je, Serikali ina mpango gani maalum wa kutangaza vivutio hivi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kutangaza vivutio hivyo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika sehemu za Newala pamoja na Mikindani na maeneo mengine ya Mtwara yana vivutio vingi vya asili, maliasili na vitu vingi kwa kweli, hivi sasa naomba niseme tu kwamba tumechukua jitihada za kuhakikisha tunatangaza vyote kwa kushirikiana na Halmashauri zilizopo katika Mkao wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatangaza maeneo yote hayo na Mji wa Mikindani tutahakikisha kwamba tunautangaza ipasavyo kwa sababu una historia ndefu na nzuri ambayo nina uhakika watalii wengi watavutiwa kwenda kutembelea katika hilo eneo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Mlata halafu Mheshimiwa Mariam Kisangi.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mikoa ya Singida, Simiyu, Tabora na Shinyanga pia ina vivutio vyake; ukienda utakutana na akina Mtemi Chenge, Chifu Mayenga, Mtemi Gerege na wengine wengi.

Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutembea mikoa hiyo ili tumwonyeshe vivutio hivyo aweze kuviiingiza kwenye ramani ya utalii kwenye mikoa hiyo? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika mikoa yote alioitaja ina vitu vingi na ina historia ndefu ya utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba nipo tayari wakati wowote kuongozana kwenda kutembelea mikoa hiyo na nitaomba wakati naenda tuongozane naye ili kusudi aweze kunionesha maeneo yote hayo na Serikali iweze kuyachukua na kuyatangaza ipasavyo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam lina vivutio vingi vya utalii kama vile Daraja la Kigamboni, Hospitali ya *Ocean Road*, Uwanja wa Uhuru, Magomeni pale kuna Nyumba ya Mwalimu Nyerere, *Karimjee Hall* na Makumbusho ya Taifa. (*Makofii*)

Je, Serikali imejipanga vipi katika kulisaidia Jiji la Dar es Salaam ambao wameanza zoezi hilo la kutangaza vivutio vya utalii kulipa nguvu ili waweze kufanya vizuri zaidi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Dar es Salaam nayo ni miongoni mwa mikoa ambayo ina vivutio vingi vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, ndiyo maana tulianza na mkakati wa kuhakikisha kwamba Dar es Salaam inatangazwa na tunaanzisha vituo vyaa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshirikiana na Mkoa kuhakikisha kwamba tunaanzisha basi maalum ambalo litakuwa linatembelea vituo vyote, kuanzia pale Makumbusho, Magomeni na maeneo mengine yote aliyoyataja kwamba yanatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tutaendeleza hizi jitihada ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba lile daraja letu la Kigamboni sasa linatumika kama mojawapo ya kivutio cha utalii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Owenya halafu Mheshimiwa Willy Qambalo. (*Kicheko*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Moshi Vijijini Kata ya Mbokomu, tumekuwa tukizungumza mara nydingi kwamba kuna mti mkubwa sana ambao ni kivutio cha utalii pale; lakini Serikali haijachukua jitihada zozote kwenda kuutangaza mti ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kujua Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani wa kuhakikisha wanautangaza mti ule uwe ni moja ya kivutio cha utalii katika Mkoa wa Kilimanjaro?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilikuwa sina taarifa kama kuna mti mkubwa wa namna hiyo, lakini naamini kabisa kama kuna mti mkubwa wa namna hiyo, basi itakuwa ni kivutio kizuri sana cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutachukua hatua za kuhakikisha kwamba kwanza nautembelea, lakini la pili, tuweze kuutangaza kusudi wananchi waweze kujua kwamba kuna mti mkubwa ambao ni kivutio kizuri sana katika Mkoa wa Kilimanjaro na katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo naomba niliseme, nchi ya Tanzania ni nchi tajiri sana ambayo ina vivutio vingi sana. Tukiwekeza, tutaweza kuivusha nchi hii na tutaweza kuisogezza mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tushirikiane Wabunge wote kuhakikisha vivutio vyote tunavitangaza kwa pamoja ikiwemo...

MWENYEKITI: Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: ...kwenye Instagram na Facebook mlizonazo muweke picha cha utalii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vya Kata ya Buger na TANAPA, pia Vijiji vya Lositete, Upper kitete, Silahamo na Endamagang na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imekuwa migogoro ya muda mrefu ambayo haipati utatuzi.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari baada ya Bunge hili kuja Karatu ili kuongoza majadiliano ya kumaliza mgogoro huo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika lile eneo kuna baadhi ya migogoro ambayo imejitokeza na imekuwepo kwa muda mrefu, ninaomba niseme tu kwamba niko tayari pale ambapo tutapanga ratiba vizuri mimi na wewe tuende tukaangalie, tukawasikilize wananchi ili tuone ni namna gani tunaweza kutatua hiyo migogoro iliyopo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini ni wa mwisho.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urithi mkubwa wa Taifa letu unapotea. Ngoma zetu zinapotea, lugha zetu za asili zinapotea, vyakula vyetu vinapotea. Wewe ni Chifu, unafahamu hazina kubwa ambayo Machifu walikuwa nayo, mavazi yao, vyombo vyao vya nyumbani, samani zao na vyote hivi vinaweza vikavutia utalii kwa kiwango kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni kwa nini usiwepo mkakati wa kila Halmashauri au kila Wilaya kujenga jumba la makumbusho na kwa sababu hiyo Viongozi wa Halmashauri na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kuhamasisha wananchi ili vitu vyote vya asili vikakusanya, kwanza kwa ajili ya elimu ya watoto wetu, lakini kwa ajili pia ya kuvutia utalii ikiwa ni pamoja na kuleta mashindano ya ngoma za asili ambazo zina mafunzo mengi sana kwa Taifa letu? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge mzuri sana ambaye amekuwa akifuatilia sana mambo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme tu kwamba kama ulivyosema ni kweli kabisa tunayo mikakati mingi ambayo tunataka kuitekeleza. Lakini kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa utaratibu wake aliyoanzisha wa kuhakikisha kwamba anashindanisha ngoma za asili, na hili ndilo tunalolitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi katika mkakati wa kuhakikisha kwamba hili tunalitekeleza, tumeamua kwamba mwezi wa Septemba kila mwaka, nchi ya Tanzania Mikoa yote, Halmashauri zote, zitakuwa zinasherehekea Mwezi wa Urithi wa Utamaduni wetu. Kwa hiyo, ngoma mbalimbali zitashiriki katika Kanda, katika Mikoa, kuhakikisha Watanzania wanakumbuka utamaduni wao. Nami ninaamini kabisa tukitekeleza hili kwa pamoja basi vitu vyote vile, mali kale zote zitawenza kubainishwa na kuweza kuelimishwa na wananchi wote wataweza kuvibaini vizuri kabisa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na swalii letu la mwisho la leo linatoka kwa Mheshimiwa Ally Seif Ungando Mbunge wa Kibiti.

Na. 404

Ujenzi wa Gati Eneo la Nyamisati

MHE. ALLY S. UNGANDO aliluliza:-

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Nyamisati wamekuwa wakipata adha kubwa sana katika eneo la kivuko.

Je, ni lini Serikali itajenga Gati la Nyamisati?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Self Ungando, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Gati la Nyamisati umeanza tangu tarehe 16 Machi, 2018 baada ya mkandarasi *M/s Alpha Logistics Tanzania Ltd.* na *M/s Southern Engineering Company Ltd.* kukabidhiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) eneo la mradi toka tarehe 2 Machi, 2018. Kazi ya ujenzi wa gati hili zinatarajiwा kukamilika katikati ya mwezi Machi, 2019 kwa gharama ya jumla ya shilingi billioni 14.435.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizofikiwa mpaka sasa hivi ni kufanya upimaji wa bahari (*bathymetric survey*), uchunguzi wa udongo (*geotechnical investigation*) katika sehemu ya kujenga gati na usafishaji wa eneo (*site clearance*). Pia mkandarasi anaendelea na maandalizi (*mobilization*) kwa ajili ya kuanza kazi rasmi baada ya kazi hizi za awali za upimaji kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya kazi hii kumekuwa na changamoto kadhaa kama vile mwingiliano wa vyombo vinavyotumia kivuko na vile vya mkandarasi. Mfano, *vessel* inayofanya kazi ya uchunguzi wa udongo inaingiliana na vyombo vya usafiri, changamoto hii inatatuliwa kwa kujenga gati la muda (*temporary berth*) kwa ajili ya kuhudumia wasafiri.

Aidha, wananchi waliokuwa wanatumia gati la zamani ambalo sasa linajengwa jipya katika eneo hilohilo walikuwa hawataki kuhama, hata hivyo, uongozi wa Wilaya umefanikisha wananchi hao kuhama lakini wanahitaji wajengewe choo katika eneo jipya la kufanya biashara walilohamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPA* tayari wanaendelea na taratibu za kujenga choo hicho cha umma ambapo mpaka sasa wapo kwenye hatua za kumpata mkandarasi wa kujenga choo hicho.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ungando.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya swali hilo, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Wananchi wa Nyamisati walipisha ujenzi huo lakini sehemu waliyopelekwa miundombinu yao imekuwa siyo rafiki. Mfano hakuna choo, banda la abiria ni kifusi katika hilo gati la muda. Je, lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi huo?

(ii) Vijana wa maeneo hayo wamejiunga na vikundi vyao vyta ujasiriamali kama mkombozi. Je, sasa Serikali ina mpango gani wa kuwapa kipaumbele katika ujenzi huo ili vijana hao wafaidike, wapate vibarua ukizingatia watu wa Pwani wanasema mgeni njoo mwenyeji apone? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ungando kwa jinsi alivyofuatilia kwa muda mrefu sana ujenzi wa gati hili la Nyamisati. Ninakumbuka kuna kipindi fulani tuliwahi kwenda naye mpaka kufanya kikao na watu wa *TPA* kwa ajili ya kufuatilia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kujibu swali lake la kwanza, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, tayari *TPA* wanamatafuta mkandarasi kwa ajili ya kujenga choo cha umma pamoja na sehemu ya kupumzika kwa maeneo ambako wananchi wamepisha ujenzi wa gati uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo, tutakapopata mkandarasi hilo eneo litajengwa kwa ajili ya wananchi kupumzika vilevile kutakuwa na maeneo rafiki kwa ajili ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wananchi ambao watakuwa wanasubiri huduma za gati hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la swali lake la pili, ninaelekeza *TPA*, ninajua kwamba kwenye mkataba ambao wameingia na hawa wakandarasi wawili kuna kipengele ambacho kinawataka wakandarasi wachukue wazawa katika shughuli zile ambazo siyo za kitaalam kuweza kufanya kazi kama vibarua na vitu kama hivyo. Ninawaagiza *TPA* wahakikishe wanafanya kazi kama walivyoingia mkataba na wakandarasi kutumia wazawa katika shughuli ambazo siyo za kitaalam. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Maryam Msabaha.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba mkandarasi yupo *site*, lakini kasi ya *mobilization* na vifaa duni anavyovitumia vinatia mashaka sana kama mkandarasi anaweza akamaliza kazi hii katika muda uliotajwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari baada ya kikao hiki cha bajeti, mimi, Mheshimiwa Ungando, Mbunge wa Kibiti na mama yetu Mheshimiwa Salma Kikwete ambaye ni mdau mkubwa sana wa Gati la Nyamisati, tufanye ziara ya pamoja ili kuhakikisha kwamba gati hili linakwisha kwa muda uliopangwa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini mtaenda huko?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba kati ya Wabunge ambao wamekuwa wakifuatilia suala la Gati hili la Nyamisati ni pamoja na Mheshimiwa Dau na Mheshimiwa

Mama Salma Kikwete, wote kwa pamoja wamekuwa wakifuatilia na wakitaka kujua hatua mbalimbali ambazo zinaendelea katika ujenzi wa gati hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vifaa wakandarasi wanavyo, bado wanaendelea kukusanya, kama nilivyozungumza kwenye majibu ya awali kwamba wako kwenye *mobilization* kwa hiyo vifaa bado vinaendelea kuletwa na wana vifaa vya kutosha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo, ndiyo maana tumeweka *deadline*, huu mradi utakabidhiwa mwezi mapema Machi mwakani. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba vifaa vitafika kwa wakati na nipo tayari kwenda nao Waheshimiwa Wabunge wote kwa ajili ya kwenda kuukagua mradi huo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kisiwa cha Izumacheri hawana usafiri tofauti na usafiri wa Meli ya *MV Chato*, leo ni mwaka wa tatu toka tumeingia Bungeni Mheshimiwa Rais aliahidi, meli hiyo inapaki juu ya jiwe, na ni mwaka wa pili tunaahidiwa kuletewa pesa kwa ajili ya ujenzi wa gati.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuambatana nami baada ya Bunge kwenda kuona adha ya meli inayo-parkuju ya jiwe ili uweze kuachia pesa kwa ajili ya ujenzi wa gati hilo?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer Nditiye*, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Rais aliahidi ujenzi

wa gati kwa eneo hilo na bado Serikali inatambua na inaendelea kufuatilia namna ya utekelezaji wa ahadi hiyo ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaaagiza *TPA* toka mwaka jana mwanzoni, wanaendelea na utaratibu wa kutuletea gharama halisi za kutengeneza gati eneo hilo ili wananchi waweze kupata huduma kwa usahihi. Nieleze tu kwamba niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Musukuma kwenda kuangalia eneo hilo kwa ajili ya kuweka gati. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Maryam Msabaha.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali la nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vivuko vyta Kigamboni vimekuwa vikiharibika mara kwa mara; je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha inavitengeneza vivuko hivi ili kuondosha maafa yasitokee kwa wananchi ambao wanavitumia?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *TEMESA* Serikali imeendelea kuvihudumia vivuko mbalimbali vilivyopo nchini kwetu kuhakikisha vinafanya kazi kama vinavyotakiwa.

Mimi nina taarifa kwamba hicho kivuko kilikuwa na hitilafu kidogo na ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kufuatilia baada ya muda, hata tukitoka nje tutawasiliana na watu wa *TEMESA* kuona kuna changamoto gani kwenye hicho kivuko ili ziweze kutatuliwa. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa kutupatia Kivuko cha Msinjahili, Kitumbikwera kule Lindi. Je, ni lini Serikali itakamilisha eneo la kituo cha kupumzika wasafiri au cha kusubiria wasafiri katika Msinjahili na upande wa Kitumbikwera? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni kweli kwamba tumerekebisha kivuko alichozungumza Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli sasa hivi kimeshaanza kutumika. Kwenye *package* ya tenda aliyopata mkandarasi wa kujenga kivuko kile, tulimwambia aweke na sehemu ambako wananchi watapumzika. Nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafuatilia kuona kwamba sehemu ya kupumzika inatengenezwa.

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mwongozo.

MWENYEKITI: Tuvumiliane tu nitafika kwenye hatua hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni tulio nao leo hapa ni wageni wa Mheshimiwa Spika waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, leo tarehe 8 Juni, ni wafuatao; Profesa Florens Luoga - Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; karibu sana Gavana. Tunaye Dkt. Ngaling'wa Balele - Msaidizi wa Gavana, tunaye pia Ndugu Yahya Mchujuko - Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Uendeshaji wa Benki Kuu, tunaye Isaac Kihwili - Mwanasheria wa Benki Kuu, tunaye Ndugu Leonard Mkude - Meneja wa Bajeti Benki Kuu, tunaye Dkt. Badria Guma - Meneja wa Huduma za Matibabu, tunaye Ndugu Zaria Mbeho - Meneja wa Uhusiano na Itifaki Benki Kuu, tunaye Dkt. Florian Vedasto - Daktari wa Benki Kuu na

tunaye Richard Wambali - Mkurugenzi wa Tawi la Benki Kuu hapa Dodoma, karibuni sana wageni wetu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii pia kwenye Jukwaa hilo la Spika pia ni wageni 19 wa Mheshimiwa Naibu Spika Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mbeya, ambao ni Wanachama wa Umoja wa Maendeleo Simike (UMASI) kutoka Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Ndugu Albert Mwaheleja, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambaao ni wageni kumi wa Mheshimiwa Hawa Ghasia Mbunge ambaao ni wanafunzi tisa kutoka Chuo cha Agha Khan kilichopo Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalimu wao Profesa Peter Kajoro, karibuni sana wageni wetu. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Willy Qambalo Mbunge ambaao ni marafiki zake kutoka Karatu Mkoani Arusha, Ndugu Pius Phirmin na Ndugu Febronia Patrice, karibuni. (*Makof*)

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Mwatumu Dau Haji Mbunge ambaao ni wajukuu zake kutoka Mjini Magharibi Ndugu Salma Mohamed, Ndugu Daliha Abdul na Ndugu Hadija Mohamed. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Leah Komanya Mbunge ambaye ni dada yake kutoka Meatu Mkoani Simiyu, Mwalimu Cecilia Tegile. Karibu sana Mwalimu Tegile. (*Makof*)

Wapo pia wageni watano wa Mheshimiwa Vicky Kamata Mbunge ambaao ni Mchungaji Sabina Gear wa Kanisa la *Deliverance Restoration Ministry* la Mjini Arusha na watoto wanne wa rafiki yake, karibuni sana. Pia kuna wageni 30 wa Mheshimiwa Augustino Masele Mbunge ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ernest Edward, karibuni sana wanafunzi. (*Makof*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk (Mbunge) ambao ni familia yake wakiongozwa na Mke wake mpenzi Ndugu Rukia Bakari. (*Makofî*)

Mgeni wa Mheshimiwa Yosepher Komba (Mbunge) ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoa wa Lindi Ndugu Daudi Faida. Wageni 16 wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Wilaya ya Kaliua, Mkoani Tabora wakiongozwa na Ndugu Amina Msambya, karibuni sana. (*Makofî*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Ungando (Mbunge) ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Ushauri la Usafiri wa Nchi Kavu na Majini kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Saidi Hamisi Puta, karibu sana. (*Makofî*)

Wageni 48 wa Mheshimiwa Dunstan Kitandula (Mbunge) ambao ni wanafunzi 41 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi ya St. Joseph Millennium ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofî*)

Mgeni wa Mheshimiwa Sixtus Mapunda (Mbunge) ambaye ni mwandishi TV1 Jijiji Dar es Salam, Ndugu Hajira Kondo, karibu sana. Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Saed Kubenea (Mbunge) ambaye ni Ndugu yake kutoka Jijini Mwanza Ndugu Joseph Makala, Ndugu Makala karibu sana. (*Makofî*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 100 na walimu watatu kutoa Chuo cha Maendeleo Dodoma (*TRACDI*), mko wapi ,haya ahsanteni popote mlipo. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine nianze na hili refu sana, Mwenyekiti wa *TWPG*, Margaret Simwanza Sitta (Mbunge) anawatangazia kwamba katika kutatta changamoto kadhaa zinazomkabili mtoto wa kike nchini ikiwemo ukosefu wa vyoo bora, Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania umekusudia kuchangisha fedha zitakazosaidia kuboresha mazingira ya mtoto wa kike

mashulenii kama ukosefu wa vyoo bora. Hivyo *TWPG* inakusudia kujenga vyoo ambavyo baada ya ujenzi huo ndivyo vitakuwa vyoo vya mfano katika ujenzi kwa maeneo yote ya shule na taasisi zote za umma nchini.

Aidha, katika kutekeleza wazo hilo imekusudiwa kujengwa vyoo vya mfano katika majimbo yote 264 ya uchaguzi nchini ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.5 zitahitajika. Hivyo njia mbalimbali zimebuniwa ili kuweza kupata fedha hizo, mionganii mwa njia hizo ni zoezi la kuosha magari ambapo fedha zitakazopatikana zitatumika katika ujenzi. Mheshimiwa Spika wa Bunge letu ataongoza zoezi hilo. Waheshimiwa Wabunge wote wanawake kwa wanaume mnaombwa kumuunga mkono Mheshimiwa Spika ili kuchangisha fedha hizo...

Waheshimiwa tusikilizane, Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane tu, nawasikia hapa vizuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yatatolewa katika Mji mzima wa Dodoma ili wananchi wajitokeze kuleta magari yao yaoshwe. Uoshaji wa magari utaanza saa 4:00 asubuhi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kujitokeza kwa wingi katika uwanja wa Jamhuri, mlele magari yenu ya marafiki zenu na pia mtusaidie kuhimiza watu wengine kujitokeza kwa wingi. Hili ni tangazo la leo, kesho saa 4:00 asubuhi, tumuunge mkono Spika wetu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba niwatangizie Wabunge kwamba kwa mujibu wa maelezo ya Meneja wa *TANESCO* Mkoani Dodoma hali ya kukatika katika kwa umeme kwenye Ukumbi wa Bunge leo inatokana na hitiflu kwenye Gridi ya Taifa ambayo imesababisha hali hiyo kutokea karibu nchi nzima. Kwa sasa wataalam wetu hapa Ofisi ya Bunge wameamua kuzima kabisa mfumo unaotoa umeme kutoka Gridi ya Taifa na badala yake wanawasha kangavuke ili kukabiliana na kukatika katika huko, kangavuke ni jenereta.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania Mheshimiwa Margaret Sitta Mbunge, anawatangazia Wabunge wote waliojiandikisha kufanya maonesho, nyimbo, kucheza, ucheshi na sarakasi kwa ajili ya siku ya tafrija ya changizo tarehe 22 Juni, 2018 kuwa leo tarehe 8 Juni, mazoezi yataendelea Saa Saba Mchana katika Ukumbi wa Msekwa C, mnaombwa mliojiandikisha kuhudhuria.

Pia Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania anawatangazia Wabunge wote wa Chama hicho kuwa leo tarehe 8 Juni, 2018 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge Wanawake wote, semina hiyo itafanyika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kuahirisha kikao cha Bunge asubuhi hii, mnaombwa mhudhurie semina hiyo, lakini ni ya wanawake tu na sisi tutafute ya wanaume. (*Kicheko*)

Mheshimiwa William Ngeleja - Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwamba siku ya kesho Jumamosi tarehe 9 Juni kutakuwa na mechi katika *Bunge Sports club (Ndugai Boys)* na *combine* ya Waganga wa Jadi na Albino saa 10:00 jioni Uwanja wa Jamhuri Dodoma. Pia siku ya Jumapili kutakuwa na mechi kali kati ya *Bunge Sports Club (Ndugai Boys)* na *combine* ya *Rorya Veteran football* na *netball* itakayofanyika katika uwanja wa Jamhuri Dodoma kuanzia saa 9:00 alasiri, Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kwenye mechi hizo.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu kwa leo ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Ngoja nikae kwanza, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Nkamia, nahama.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Sophia.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Bobali.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: *Gender Sophia.*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Mwakajoka, Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: *Gender Sophia.*

MWENYEKITI: *Gender inaingiaje katika Mwongozo? (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwakagenda tunaanza na wewe.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo na nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, alipomuuiliza swali juu ya fedha shilingi bilioni 200 za Zanzibar, Naibu Waziri ameonesha mkanganyiko kutokana na ripoti aliyoitao katika Bunge lako tukufu kipindi cha bajeti ya Wizara yake. Ninaomba ufanuzi wa Bunge na yeze Waziri atueleze Wabunge ni kipi tukiamini na ni sahihi, kati ya ripoti aliyoitao katika Bunge lako tukufu au jibu alilomjibu Mheshimiwa Khatib Said Haji. Kipi ni sahihi tunahitaji kujua ili tuweze kukihamini na wananchi wetu wakakihamini. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata Mwongozo wako, nimesimama kwa kanuni ya 68(7); wakati Mheshimiwa Ruth Mollel, anachangi kwenye swali lake amesema viongozi wengi, Wakurugenzi walioko kwenye Halmashauri walikuwa

ni wanachama wa CCM. Ninataka kupata Mwongozo wako kwamba cheo cha Mkurugenzi ni cheo kidogo sana, muuliza swali alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara, lakini leo ni mwansasiasa. Wakati tukifanya uchaguzi alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara, sasa ni Mbunge wa CHADEMA.

Je ni sahihi yeye kuwa CHADEMA wakati alikuwa Mtendaji wa Serikali?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru name nitumie Kanuni ya 68(7) kutokana muda nisingependa niupoteze na wala nisiosome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Joseph George Kakunda akijibu swali la *Engineer* Edwin Amandus Ngonyani, linalouliza juu ya Serikali ya Awamu ya Nne kwamba ilihaidi kuanzisha Mkoa mpya wa Selous.

Nilikuwa naomba mwongozo wako, Tanzania hii ni kubwa Wabunge wengi hapa ndani tumekuwa nikiwemo mimi tumekuwa tukiuliza juu ya mgawanyo wa Majimbo, Wilaya na hata Mikoa kwa muda mrefu. Wengi tumekuwa tukitaka Wilaya zetu zetu zigawanywe au Majimbo yetu yagawanywe kutokana na ukubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa tathmini ndogo tu ambayo nimeifanya yapo Majimbo mengine ni makubwa sana na yapo Majimbo mengine yana Kata saba, nane, sita na watu hao hao wanapata *equal share* ndani ya Bunge, kunakuwa na kitu kina unaweza kusema *unbalanced division of the nation cake*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa haioni kwamba kabla ya kugawanya Wilaya, Mikoa na Majimbo ifanye kwanza tathmini upya ya majimbo yaliyopo na Wilaya zilizopo na mikoa ili yopo, kabla ya kugawanya ili kuwe na haki katika Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kabla ya kugawa majimbo hata llikwemo la Chemba ifanye kwanza tathmini upya, siyo vizuri Mbunge mmoja anakuwa na kata sita mwingine ana kata 38 halafu mnakuja humu ndani mnapata *equal share* hata ya kuchangia kwenye bajeti, sidhani kama ni sahihi sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa Mbunge.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba jambo hili kabla ya kugawa Majimbo na Wilaya kwanza tuangalie. Je, kulikuwa na haki ya kugawa baadhi ya maeneo au ni watu walitafutiwa nafasi tu? Ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nassari.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 47 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 48 kwa maana ya masharti ya jambo lenyewe ambalo nitalisema kwenye Kanuni ya 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu haya nitatoa hoja na nitaomba Waheshiwa na hususani Wabunge Wanawake ambao mko ndani ya Bunge hili mniunge mkono. Ukitumba Katiba ya Jamhuri Ibara ya 63(2) inasema kwamba; "Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwana madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano..."

MWENYEKITI: Mheshimiwa, nisomee Kanuni tu usiniletee hayo mengine.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 47 ni ndefu....

MWENYEKITI: Basi nenda *straight* tu usinisomee hayo.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya juzi tarehe 6 Juni, mwaka 2018 huko Mang'ula Wilayani Kilombero, Mkoani Morogoro, mama mmoja ambaye alikuwa ni mjamzito wa kujifungua, Mtanzania huyu ambaye alikuwa amefika hatua za kupewa kichanga chake alishikwa na polisi kwa sababu ambazo zimedaiwa kwamba hapakuwa na makosa, lakini akawekwa ndani polisi mahabusu na akawa anajisikia uchungu wa kutaka kujifungua kichanga chake. Aliwaeleza polisi wale hali aliyokuwa nayo na hata bila kuwaeleza ilionekana ni hali ya namna gani. Lakini polisi walimng'ang'ania na mpaka hatua ya mwisho ilipofika ya yule mama kuanza kudhalilika akiwa ndani ya mahabusu akaanza kutoka na maji kujifungua kichanga kile ndipo polisi walipomruhusu akatoka nje na matokeo yake akajifungua mtoto wake nje, chini kwenye nyasi na mchanga kama mnyama, bila msaada wa mtu yejote.

Matukio kama haya yamejitokeza siku za nyuma na imekuwa kama ni *trend ya police brutality*, pengine tunaona vitu vingine vinakwenda kwenye siasa, lakini kwa wanawake na hususani wanawake ambao watoto wachanga ama ni wajawazito ama wanakaribia kujifungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ilitokea mama mmoja akiitwa Elizabeth...

MWENYEKITI: Endelea tu umemaliza, nimekuelewa endelea tu sitaki hotuba, nawaombeni sana.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga tu hoja hili kwa sababu naomba kuungwa mkono.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tunapoteza muda tu.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sasa kwa sababu lilitokea tukio kama hili Dar es Salaam....

MWENYEKITI: Unafahamu...

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, limetokea Mwanza...

MWENYEKITI: Unabishana na mimi *for nothing*...

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *thank you, I go straight to the...*

MWENYEKITI: Mimi ndiyo naongoza, dharura hajji namna hiyo Mheshimiwa Nassari, dharura hiyo ni lazima iwe imetokea leo. Tusibabaishane na hilo, naendelea wewe haupo kwenye dira. Ni tukio la hovyo hata mimi nakubaliana na wewe, lakini Mwongozo wangu kwa hilo halipo, ahsante, usiendelee. Serikali imesikia watafuatilia, lakini halikutokea hapa Bungeni. Tunaendelea Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo. Nimesimama kwa Kanuni 68(7) kwa jambo ambalo limetokea Bungeni. Jana wakati Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Vunjo...

MWENYEKITI: Nakuomba ukae chini tu Mheshimiwa, nakuomba tu ukae chini halijatokea mapema leo. (*Kicheko*)

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana ilizuiwa na hili jambo linahusu haki za Bunge.

MWENYEKITI: Nimetoa maelekezo yangu Mheshimiwa Kubenea, hili halijatokea mapema leo. Umesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) ungelisimama kwa Haki za Bunge ni Kanuni tofauti. Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimesimama kwa Kanuni ya 47 kwenye Haki za Bunge.

MWENYEKITI: Kanuni gani?

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 47 pamoja na Kanuni ya 50 Haki za Bunge, zote kwa pamoja.

MWENYEKITI: Huwezi kuchanganya zote, *no*, semea moja tu hiyo. (*Kicheko*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ni Kanuni ya 51. Niendelee kutoa hoja au niisome.

MWENYEKITI: Hebu isome Mheshimiwa. (*Kicheko*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 51(1) Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na Haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge ulliowekwa na Kanuni hizi na atakuwa amemuarifu Spika mapema...

MWENYEKITI: Aaha! (*Kicheko*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mmeniingiza chaka ninyi (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara hebu kaa tu, naomba ukae basi.

Waheshimiwa Wabunge, ndio maana nilitaka na ninyi mumsikilize asije akasema mimi nimem-*rule out of order* kwa kumuonea, hapana! Ukitaka kutumia Kanuni hiyo lazima uwe umeniandikia mapema hapa, huwezi ukasimama tu unasema na mimi nipime wakati umeniletea niweze kupima kama kweli inagusa Haki ya Bunge. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wafanyabiashara katika nchi hii kwa

kitendo ambacho kinaendelea sasa hivi kwamba wafanyabiashara wote nchini wanatakiwa kufungua biashara zao siku ya Jumamosi baada ya saa nne asubuhi. Jambo hili limesababisha usumbufu mkubwa na limesababisha kukosekana kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali pia. Serikali ina mpango gani wa kutoa tafsiri sahihi kuhusiana na siku ya usafi kwa sababu badala ya usafi huu kufanyika kila siku ya Jumamosi ya wiki basi jambo hili lingekuwa linafanyika hata mara moja kwa mwezi.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na usumbufu wa hali ya juu sana na wananchi wanalamika sana, wafanyabiashara wanashindwa kufungua biashara zao kwa muda muafaka.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) pamoja na kanuni ya huruma yako kutokana na yanayowakuta Watanzania wenzetu ambao wamekamatwa nchini Kenya ambao ni wavuvi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania 109 ambao wamekamatwa katika Bahari ya Hindi, ufukweni katika maeneo ya Moa, Wilaya ya Mkinga. Pia jana usiku kimekamatwa chombo cha mizigo kikiwa na wavuvi, wote hawa ni Watanzania wamepelekwa Kenya na wako mahabusu sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo askari wetu wa *Navy* ambao wanafanya doria katika bahari yetu, wao wanafanyakazi gani mpaka Watanzania wananyanyaswa ndani ya mipaka yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukumbuke wapo Watanzania...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niombe muongozo juu ya suala ambalo Mheshimiwa Nassari alishaomba mwongozo na ulishalitolea mwongozo wake.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, hoja yangu imeshapata majibu.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Selasini.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwashukuru sana kwa kuanza kuzielewa Kanuni zetu. Kuhusiana na Kanuni ya 68(7) liwe ni jambo mahsus ambalo limetokea mapema siku hiyo yaani mapema imepewa tafsiri siku hiyo hiyo, nashukuru sana kwa hayo ambayo mmeyasema.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sura hiyo hiyo, Mheshimiwa Mwakajoka umesimama kwa suala hilo, Mheshimiwa Kubenea halijatokea hapa na kama nilivyomalizia na Mheshimiwa Mbarouk, matukio haya hayajatokea hapa. Mheshimiwa Nassari nilianza mapema kukuongoza kwa hiyo ninabaki na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Joseph Musukuma na Mheshimiwa Juma Nkamia.

Mheshimiwa Mwakagenda swal la msingi liliulizwa na mwenye swal, Mheshimiwa Khatib Said Haji nilimruhusu kuuliza swal la nyongeza aauliza. Halikuwa swal lake lakini ana haki ya kuuliza swal la nyongeza kama Mbunge akajibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango majibu yanayohusiana na pesa hiyo shilingi bilioni

200 ya Zanzibar, hayo ni majibu ya nyongeza kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatib Said Haji. Mwenye swali la msingi alijibiwa na Serikali akaridhika, mwenye swali la nyongeza kajibiwa na Serikali, anaweza kuwa hakujisikia vizuri na majibu hayo.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda lakini wewe sasa unapokuja hapa Kanuni zetu zinatutaka kama hujaridhika na jibu hilo uliza swali lakini huwezi ukaliombea mwongozo. Ingekuwa mwenye swali la msingi anaamini majibu aliyopewa na Serikali hakujibiwa kikamilifu hapo ndipo yeye angeweza kusema naomba swali hili lijibiwe tungeenda kuangalia sasa kwenye *Hansard* kama kweli majibu yaliyotolewa na Serikali na baada ya kuuliza kama yamekidhi kiwango cha swali hilo.

Kwa hiyo Mwongozo wangu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ni kwamba hakuna swali ambalo linastahili mimi kulitolea Mwongozo.

Mheshimiwa Joseph Musukuma narudia tena hivyo, liliulizwa swali na Mheshimiwa Ruth Mollel aliiuliza Serikali kuhusiana na watumishi hao, likajibiwa na maswali ya nyongeza yalikuwepo yakajibiwa na Serikali tena kwa ufasaha tu, wewe hukuwa sehemu ya huyo mwenye swali la msingi. Kwa hiyo, Mwongozo wangu kwa hilo, na wewe sina kitu cha kuombewa Mwongozo wa hali hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Juma Nkamia kwa mtiririko huo huo, Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda alijibu swali la msingi na maswali ya nyongeza kuhusiana na swali hili, wewe hukuwa mwenye hoja kwa maana ya swali la msingi. Aliyejibiwa inawezekana na yeye hadhani kwamba limejibiwa kwa kiwango alichotaka yeye, lakini anachowesta kufanya ni yeye mwenyewe kuuliza au angesimama kusema kwamba swali langu halikujibiwa kama nilivyotaka mimi au kama nilivyoliuliza mimi.

Sasa wengine hawa, nisitumie neno kudandia, hapana, kuuliza maswali ya nyongeza, huwezi ukalalamika

kwamba swalı langu la nyongeza halikujibiwa kwa sababu tofauti na swalı la msingi ambalo Serikali imeenda ikafanya utafiti wake na ikalileta Bungeni, haya ya nyongeza unajibiwa kwa kutokana na uwezo wa yule anayekujibu na ndiyo maana huwa tunawashauri sana Waheshimiwa Wabunge, kuna Mawaziri wengi na Naibu Mawaziri wengi wana uwezo wa kuyajibu maswali yenu lakini hatuwatendei haki sana tunapowa-*load* na maswali ambayo mpaka kwenye vijiji vyetu wayajue wakiwa humu Bungeni lakini ya maandishi ndiyo maana Serikali inajibu kwa maandishi, wamelifanya utafiti na ndiyo maana kanuni ziko wazi kama hukujibiwa kikamilifu lazima una haki ya kusema kwamba swalı langu halijajibiwa kama nilivyokuwa nimeuliza. Huo ndiyo Mwongozo wangu kwa hayo niliyoombwa kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wa tukio la Morogoro narudia kusema kama kweli limetokea ni tukio la hovyo, tukio la kinyama na Serikali kama mna cha kusema ni vema mkayasemea humu na Taifa likasikia.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer Masauni*.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kutoa ufanuzi kuhusiana na tukio ambalo lilitokea Morogoro hivi karibuni likimhusisha mama anayeitwa Bibi Amina Raphael Mapunda ambaye alikuwa mjamzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Serikali tunaomba kutoa masikitiko yetu makubwa kuhusiana na tukio hili liliyvojiteze. Naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge hapa na wananchi wote kwa jumla kwamba jambo hili sasa hivi tayari limeshafunguliwa jalada la uchunguzi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kilichotokea kwa ufupi ambacho kilipelekea hata tuweze kulichukulia kwa uzito unaostahili hili jambo ni kwamba kulikuwa kuna tukio la wizi ambalo lilihuisha mume wa huyu mama ambaye

inasemekana kwamba alinunua moja kati ya vifaa vilivyoibiwa, vifaa vingi vya nyumbani vilibowi, yeye alinunua sehemu ya kitanda.

Kwa hiyo, baada ya wale ambao wameibiwa kutoa taarifa polisi na polisi kuchukua jukumu hilo la kwenda *ku-search* katika nyumba ambayo ilisemekana kwamba ina sehemu ya vifaa hivyo vilivyoibiwa, mhusika ambaye ni mume wa huyu mama ambaye yeye inasemekana ndiye aliyenunua hivyo vifaa ambaye anaitwa Ndugu Abdallah Mohamed hakuwepo nyumbani kwake. Polisi walimtaarifu mama huyu kwamba ni vema atakaporejea aweze kwenda polisi kwa ajili ya kulisaidia Jeshi la Polisi kufahamu undani wa jambo hili kwa sababu mali ya wizi imepatikana katika nyumba ile, lakini hakufanya hivyo. Hivyo polisi wakachukua maamuzi ya kuweza kumchukua huyu mama kwa lengo la kumhoji kwa sababu vifaa vya wizi vimepatikana katika nyumba ambayo yeye ni mhusika wa ile nyumba na nyumba ile ni ya yeye na mume wake, kwa hiyo walikwenda kumhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunadhani hakikuwa sahihi, kwamba katika mazingira ya kawaida busara ingeweza kutumika. Kwanza hali ya Mama huyu ilikuwa ni hali ambayo ni mjamzito, wangeweza wakamhoji, wakamwambia ajidhamini arudi nyumbani, ndiyo maana tukasema kwamba tumelichukua kwa uzito na tunalichunguza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujisikia uchungu wakati yuko pale ndiyo askari polisi wakafanya jitihada za kumfikisha kwenye Kituo cha Afya, lakini kwa bahati mbaya kutohama na hali ya ujauzito ilikuwa imefikia kiwango kikubwa hakuweza kufika akajifungulia pale nje ya Kituo cha Polisi siyo mbali na sehemu ile.

Kwa ujumla, Serikali tunasikitika kwa kilichotokea na tunaendelea na uchunguzi, baada ya uchunguzi huo hatua zitawezza kuchukuliwa kwa wale ambao wamehusika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa maelezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, sina kingine cha ziada. Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu Tarehe 11 Juni, 2018, saa tatu asubuhi.

(Saa 5.13 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu Tarehe 11 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)